TAARIFA YA MTENDAJI MKUU DKT. SISTON MASANJA MGULLAH KATIKA SHEREHE YA MAHAFALI YA ISHIRINI NA TANO (25) YA ADEM KWA WAHITIMU WA STASHAHADA YA UONGOZI NA USIMAMIZI WA ELIMU (DEMA) NA STASHAHADA YA UKAGUZI WA SHULE (DSI) KWA MGENI RASMI DKT. LEONARD AKWILAPO, KATIBU MKUU, WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA SIKU YA IJUMAA

TAREHE 24 NOVEMBA, 2017

Ndugu Mgeni Rasmi,
Ndugu Mkuu wa Wilaya,
Ndugu Afisa Elimu wa Wilaya,
Ndugu Wafanyakazi wa ADEM,
Ndugu Wahitimu,
Ndugu Rais wa Serikali ya Wanafunzi,
Ndugu Wanafunzi wa ADEM,
Wageni Waalikwa,
Waandishi wa Habari,
Mabibi na Mabwana.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Kwa niaba ya wafanyakazi wote wa ADEM, Wanachuo na Wanajumuia wa ADEM tunamshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kukutana tena na kuiona siku hii muhimu ya Mahafali ya 25 ya ADEM kwa Wahitimu wa Kozi ya Kozi Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (DEMA) Stashahada ya Ukaguzi wa Shule (DSI). Tunamshukuru

Mungu pia kwa kukuwezesha wewe Mgeni Rasmi kufika salama hapa Bagamoyo kwa ajili ya kufanikisha shughuli hii ya Mahafali. Napenda pia kuwakaribisha na kuwashukuru wageni wote waalikwa ambao mmeacha shughuli zenu na kukubali kuja kujumuika nasi katika Mahafali haya. Karibuni sana!

Ndugu Mgeni Rasmi,

Napenda kutumia nafasi hii kukushukuru sana kipekee kwa kukubali kuja kushirikiana na sisi ukiwa Mgeni Rasmi kwenye Mahafali haya. Tunajua una majukumu mengi ya kitaifa yanayokukabili, lakini umekuwa mwepesi wa kuja kushirikiana na sisi katika Mahafali haya. Kukubali kwako kumetupa faraja kubwa sana wana ADEM na kunakupa wewe binafsi nafasi ya kujionea mafanikio ya kazi ya Taasisi yako ukiwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Tunakushukuru sana na karibu sana ADEM.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Niwapongeze Wafanyakazi wote wa ADEM Bagamoyo, Mbeya na Mwanza kwa kazi kubwa walioifanya ya kufundisha na kulea Wanachuo na leo hii tunashuhudia matunda ya jitihada zenu. Nikiwa Mkuu wa Wakala wa ADEM nawapongeza sana!!

Ndugu Mgeni Rasmi,

Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Wahitimu waliotukutanisha hapa leo kwa kazi kubwa walioifanya kwa muda wa miaka miwili (02) na kufanikiwa kuhitimu siku hii ya leo. Tumeona na tunaheshimu jitihada zenu za kusoma kwa bidii na kufanikiwa kutunukiwa vyeti vya Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu na Ukaguzi wa Shule. Hongereni sana!

Ndugu Mgeni Rasmi,

Naomba nitumie fursa hii kuwaeleza wadau wa elimu kwamba Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) ulizinduliwa rasmi tarehe 31 Agosti, 2001 kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 30 ya mwaka 1997 ya uanzishwaji wa Wakala za Serikali. Wakala upo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Malengo ya kuanzishwa kwa ADEM ni kutekeleza azma ya Serikali ya kuboresha Uongozi na Usimamizi wa elimu nchini katika Shule za msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na kwa Maafisa elimu wote kuanzia ngazi ya Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa. ADEM pia inawajibu wa kutoa mafunzo kwa Wathibiti Ubora wa Shule ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Katika kutekeleza haya, ADEM inaendesha mafunzo ya Muda Mrefu na Mfupi kuhusu Uongozi, Menejimenti ya Elimu na Uthibiti Ubora wa Shule. ADEM pia inatoa Ushauri weledi na kufanya Tafiti juu ya Menejimenti ya elimu ili kuzishauri Taasisi na Wizara zinazosimamia elimu kuhusu kuboresha uongozi na menejimenti ya elimu nchini. Hivi sasa Wakala una matawi matatu ya kutoa mafunzo Bagamoyo, Mbeya na Mwanza.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Kama nilivyotangulia kusema kuwa ADEM inatoa mafunzo ya Muda Mrefu na Mfupi. Zipo kozi tatu hadi hivi sasa ambazo zinatolewa kwa Muda Mrefu. Kozi ya kwanza ni ile ya Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (Diploma in Education Management and Administration-DEMA) inayotolewa kwa muda wa miaka miwili. Kozi hii inalenga kuwaandaa viongozi na viongozi tarajali kuweza kupata maarifa na stadi za kusimamia elimu ngazi ya Shule, Kata na Halmashauri. Kozi ya pili ni Stashahada ya Ukaguzi wa Shule (Diploma in School Inspection) ambayo ilianzishwa mwaka wa masomo 2014/2015 ikilenga kuwaandaa Walimu kuthibiti ubora wa Shule na sekta ya Elimu kwa ujumla. Kozi ya tatu ni ya Cheti cha Uongozi na Usimamizi wa Elimu (Certificate in Education Leadership,

Management and Administration - CELMA). Kozi hii imeanza mwaka wa masomo 2014/2015 ikilenga kuimarisha usimamizi wa elimu katika ngazi ya shule. Kwasasa kozi ya CELMA inaendeshwa kwa walimu wakuu wote katka mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe chini ya ufadhili wa **UNICEF**. Jumla ya Wahitimu **860** wamehitimu masomo yao katika awamu ya kwanza mwezi Novemba 2016.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Kwa upande wa Mafunzo ya Muda Mfupi, Wakala umeweza kuendesha Mafunzo ya Uongozi na Menejimenti ya Elimu kwa viongozi wa ngazi mbalimbali za elimu nchini katika vipindi mbalimbali. Kwa mfano, Mwaka 2016/17 ADEM imetoa mafunzo ya kuimarisha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa Walimu wapatao **31,993** wa Darasa la Tatu na la Nne katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Pia kwa mwaka 2016/17 Wakuu wa Shule **1,200** wamepata mafunzo juu ya Usimamizi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Shule (Construction Management in Secondary Schools). Pia tunatarajia kuendesha mafunzo kwa walimu wanaofundisha madarasa ya MEMKWA wapatao **1,500** na kuendesha mafunzo kwa Walimu

wanaofundisha darasa la I na II wapatao **1,600** kutoka shule za msingi zenye mikondo zaidi ya miwili.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Napenda kuchukua fursa hii kuzishukuru Wizara zinazosimamia elimu nchini, tukianza na Wizara yako ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kuweza kufadhili mafunzo ya muda mfupi ambayo yameonesha kuleta mabadiliko makubwa katika nyanja ya Uongozi na Menejimenti ya Shule pamoja na umahiri katika ufundishaji shuleni. Asanteni sana.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Mbele yako tunashuhudia matunda ya Wahitimu wa Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu(DEMA) na Ukaguzi wa Shule(DSI). Wahitimu hawa wamesoma kwa bidii na leo wanatunukiwa vyeti vyao.

Wahitimu wa Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (DEMA) walianza mafunzo yao mwaka 2015/16 jumla yao wakiwa **428** wakiwemo Wanaume **230** na Wanawake **198** na leo hii wanahitimu **417(97.4%)** wakiwemo wanaume **224** na wanawake **193.** Wanachuo

11(2.6%) wameshindwa kuhitimu kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ugonjwa na matatizo ya kifamilia.

Moduli walizosoma kwa muda wa miaka miwili ni hizi zifuatazo:

a. Information Communication Technology and Computer Applications
b. Development Studies
c. Study and Communication Skills
d. Management and Administration in Educational Institutions
e. Introduction to Curriculum Development and Implementation
f. Educational Research Methods
g. Introduction to Educational Planning
h. Introduction to Financial Management
i. Educational Policy and Legislation
j. Guidance and Counseling in Educational Organizations
k. Introduction to Human Resources Management Educational Leadership
l. Economics of Education and Resource Mobilization
m. Management of Educational Funds
n. Office and Record Management
o. Educational Statistics

p. Materials Management in Education Institutions
q. Project Planning, Monitoring and Evaluation
r. Entrepreneurship Development in Educational Institutions
s. Independent Study and Field Practice
t. Management of Classroom Instruction and Assessment
u. Staff Development and Performance Management

Ndugu Mgeni Rasmi,

Kwa upande wa Wahitimu wa Stashahada ya Ukaguzi wa Shule(DSI) walikuwa **334** walianza masomo mwaka 2015/16 wakiwemo wanaume **201** na Wanawake **133** na leo hii wanahitimu **319(95.5%)** wakiwemo wanaume **191** na wanawake **128.** Wanachuo **15(4.5%)** wameshindwa kuhitimu kutokana na sababu mbalimbali kama zilizotajwa hapo awali.

Moduli walizosoma ni hizi zifuatazo:

a) Information and Communication Technology in Education
b) School Inspection and Supervision
c) Curriculum Management and Implementation
d) Study and Communication Skills
e) Methods and Techniques of Teaching 3Rs

f) Methods and Techniques of Teaching Sciences and Mathematics
g) Education Policy and Legislation
h) Methods and Techniques of Teaching Humanities
i) English Language
j) Methods and Techniques of Teaching Languages
k) Educational Research
l) History
m) Kiswahili na Stadi zake
n) Geography
o) School Development Planning and Resource Mobilization
p) School Leadership and Management
q) Guidance and Counselling in Educational Institutions
r) Introduction to Educational Statistics
s) Monitoring and Evaluation in Education Institutions
t) Quality Assurance in Schools
u) Disaster Risk Reduction in Schools
v) Staff Management and Development
w) Assessment and Evaluation of Teaching and Learning
x) Financial and Materials Management in Schools

y) Development Studies

z) Independent Study and Field Practice

Ni matumaini yetu kuwa wahitimu watatumia maarifa na ujuzi walioupata kutoka katika moduli zote walizosoma katika kuboresha utoaji wa Elimu shuleni.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Kiwango cha ufaulu wa Wahitimu wa kozi ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu(DEMA) unaonesha kuwa wahitimu **97(23.3%)** wamepata Daraja la Kwanza, wahitimu **272(65.3%)** wamepata Daraja la Pili la Juu, Wahitimu **46 (11%)** wamepata Daraja la Pili la Kawaida na wahitimu **2(0.4%)** wamepata Daraja la Kawaida.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Kiwango cha ufaulu kwa upande wa Wahitimu wa Kozi ya Ukaguzi wa Shule (DSI) unaonesha kuwa wahitimu **66(20.6%)** wamepata Daraja la Kwanza, wahitimu **223(70%)** wamepata Daraja la Pili la Juu, Wahitimu **30(9.4%)** wamepata Daraja la Pili la Kawaida na hakuna mhitimu aliepata Daraja la Kawaida.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza wahitimu wote kwa ufaulu mzuri. Hii ni ishara kwamba wahitimu hawa wameiva na wako tayari kwa kazi. Naomba pale nafasi zinapopatikana wapewe kipaumbele katika uteuzi wa nafasi za Uongozi na Uthibiti Ubora wa Shule wa juu zaidi kutokana na sifa ya taaluma na utaalamu waliopata.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Katika kuboresha utendaji kwa wahitimu wetu, ADEM imefanya mapitio ya mtaala kwa kuongeza baadhi ya masomo ya kufundishia kwa walimu wanaosoma Stashahada ya Uongozi na Menejimenti ya Elimu. Masomo hayo ni Hisabati, Jiografia, Historia, Kiswahili na Stadi zake na Kiingereza. Hii ni hatua muhimu katika mageuzi ya kifikra kwa wahitimu wetu. Tunaamini kuwa Kiongozi mzuri ni yule anayekuwa na uelewa wa kazi na umahiri unaohitajika katika kutenda kazi fulani. Kuingiza masomo ya kufundishia katika mtaala kutamsaidia mhitimu wetu kufanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za ufundishaji kwa weledi mkubwa.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Katika kuboresha huduma na kufikia malengo yake, ADEM inakusudia kufanya yafuatayo:

- Kuboresha vituo vyake vya Bagamoyo, Mwanza na Mbeya ili kuweza kutoa mafunzo ya Uongozi wa elimu kwa wadau wengi zaidi na kwa ubora zaidi.
- Kufanya tafiti nne juu ya Uongozi na uendeshaji wa elimu.
- Kushirikiana na Wadau wa Elimu wa ndani na nje ili kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi.
- Kuajiri Wakufunzi na Wafanyakazi mahiri wa ADEM wa kada mbalimbali kadiri bajeti ya Serikali itakavyoruhusu ambao watatumika kuendesha mafunzo ya Uongozi na Uthibiti Ubora wa Shule.
- Kuwajengea uwezo wafanyakazi kupitia mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi ili wawe mahiri zaidi katika utendaji wa kazi zao.
- Kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu ya chuo.
- Kuendelea na maandalizi ya Mtaala wa Shahada ya Uthibiti wa Ubora wa Shule.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Tunaiomba Wizara yako itusaidie katika maeneo yafuatayo:

- Kutengewa fedha ya kutosha ya kukarabati jengo kubwa liliokuwa la Mapadri (Fathers House),
- Kutengewa fedha ya kutosha ya Kukarabati Mabweni ya wanachuo pamoja na kujenga Ukumbi mkubwa wa Mhadhara (Lecture Theatre) wenye uwezo wa kukaa wanachuo mianne.
- Kuendelea kutengewa nafasi za ajira mpya ili kukidhi ikama katika kampasi zote tatu.
- Kuwapa kipaumbele katika Uteuzi wa nafasi mbalimbali za Uongozi na Utendaji Wahitmu wa ADEM wa kozi za Uongozi na Uthibiti Ubora wa Shule.
- Kuweka Sera au Maagizo rasmi kwamba Uteuzi wowote wa Uongozi katika elimu na Uthibiti Ubora wa Shule utokane na Taaluma ya Uongozi na usimamizi wa elimu na uthibiti ubora wa shule.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Tumawapongeza viongozi wetu kwa jitihada mnazochukua katika kuboresha mifumo ya utoaji Elimu nchini. Tumeshuhudia mabadiliko makubwa juu ya uboreshaji mitaala ya Elimu ambapo baada ya maboresho hayo Walimu wanaofundisha darasa I - IV wamepata mafunzo ya

namna ya kuimarisha ufundishaji wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Zaidi ya hapo tumeshuhudia pia maboresho katika maandalizi ya walimu na hasa uboreshaji wa miundombinu ya vyuo vya ualimu na kozi za ualimu nchini. Vilevile tuomeona maboresho ya utoaji mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu nchini kwa kutaja machache.

Tunaendelea kuwaombea kwa Mwenyeji muendelee kuwa na afya njema na maisha marefu ili muweze kutimiza majukumu mliyopewa na Mheshimiwa Rais pamoja na Wanacnhi wote katika kutoa Elimu Bora nchini. Mbarikiwe sana!!

Ndugu Mgeni Rasmi,

Naomba nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kutimiza miaka miwili madarakani ambapo tunashuhudia mageuzi makubwa katika sekta ya Elimu, uimarishaji miundombinu ya Barabara, reli na usafiri wa Anga, mapambano dhidi ya Rushwa na kuimarika kwa Usalama na Amani nchini. Tunamuahidi kufanya kazi kwa bidii ili kuliletea taifa la Tanzania maendeleo makubwa na endelevu. Nasi tuko pamoja katika kuboresha elimu kwa kutoa mafunzo ya Menejimenti na Uongozi na Uthibiti wa

Ubora wa Shule nchini. Sisi sote kwa ujumla wetu tunaunga mkono kauli mbiu ya HAPA KAZI TU!

Ndugu Mgeni Rasmi,

Naomba nitumie fursa hii kuwaasa wahitimu kwamba msiende kubweteka na elimu hiyo ya Stashahada (Diploma) bali mkaendelee kuitafuta elimu zaidi na zaidi. Kwa sasa nafasi za uteuzi pamoja na mambo mengine yanazingatia kiwango cha elimu ya mteuliwaji. Baada ya miaka kadhaa tukikutana tutaulizana uko wapi sasa hivi, maana yake una kiwango gani cha elimu? Umuhimu wa elimu unasisitizwa hata kwenye vitabu vitakatifu kwamfano katika Biblia ukisoma kitabu cha Mithali 4:13 inasema mshike sana elimu usiacha aende zake, maana ni uzima wako na katika Quran Takatifu inasema mtafute sana elimu mpaka nchi za mbali na mpaka Uchina. Hivyo, mjitahidi kujiendeleza zaidi na zaidi ili mfikie viwango vya juu vya elimu.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Nimalizie kwa kukushukuru kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika Mahafali haya. Pia nirudie kuwapongeza Wahitimu wote kwa mafanikio waliopata. Niwashukuru pia wageni wetu wote waliojumuika nasi siku hii ya leo.

Niwatakieni kila la heri katika shughuli hii maalum ya kuwatunuku vyeti Wahitimu wa DEMA na DSI leo hii.

MUNGU IBARIKI AFRIKA,

MUNGU IBARIKI TANZANIA,

MUNGU IBARIKI ADEM,

Asanteni sana Kunisikiliza